



## **TAMKO KUHUSU KUTOWEKA KWA MWANASHERIA TITO MAGOTI**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umesikitishwa na taarifa za kutoweka kwa Mwanasheria na mfanyakazi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ndugu Tito Magoti.

Tito Magoti ni Mtetezi wa Haki za Binadamu ambaye pia ni Afisa programu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambaye amechukuliwa kwa nguvu na watu Watano maeneo ya Mwenge kituo cha mafuta cha Puma na kisha kutokomea naye kusikojulikana.

Katika tukio hilo lililotokea asubuhi ya leo, watu hao walitumia nguvu kumuingiza Tito kwenye gari aina ya Harrier wakiwa wamevalia mavazi ya kiraia. Jitihada za kumtafuta ndugu Tito Magoti katika vituo mbalimbali vya polisi zinaendelea.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umesikitishwa sana na tukio hilo kwani matukio kama haya yameendelea kushamiri haswa kwa Watetezi wa Haki za Binadamu.

Tunaliomba Jeshi la Polisi kuchukua hatua za haraka na za maksudi kuhakikisha Mtetezi huyu anapitakana akiwa salama.

Tunawaomba watetezi, wanahabari na wananchi wote kwa ujumla tuungane na kupaza sauti zetu kwa ajili ya ndugu Tito Magoti.

Imetolewa na:

Mratibu Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)  
Leo tarehe 20/12/2019

### **Board of Directors:**

Ms. Vicky Ntetema, Michael Kyande, Kenneth Simbaya, Deogratius Nsokolo, Maxence Melo, Christina Kamili, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko.

*Defending Human Rights is not a Crime!*